# "ULEMAVU BARANI AFRIKA"
## EPISODE 8: "Siyo rahisi hivyo"

**AUTHOR: Chrispin  Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt , Aboubakary Liongo**

**List of characters / episode 8:**

MSIMULIZI

**<u>SCENE ONE: OUTSIDE KAREMI'S HOMESTEAD</u>**

- Oluanda (mume, 18)
- Zabibu (mke, 15)

**<u>SCENE TWO : BREAK-TIME AT SCHOOL</u>**

- Kangwa (mke, 18)
- Chitoto (mume, 19)
- Bi. Nina (mke, 45)
- Karemi (mume, 18)

**<u>SCENE THREE : AT MAGANYE POLICE STATION</u>**

- Oluanda (mume, 18)
- Gidi (mume, 38)
- Inspekta Joe (mume, 30)

**<u>SCENE FOUR: OUTSIDE OLUANDA'S HOME</u>**

- Oluanda (mume, 18)
- Kangwa (mke, 18)
- Bw. Mali (mume, 50)

**UTANGULIZI:**

Hujambo na karibu katika Noa bongo,jenga maisha yaok. Hiki ni kipindi cha nane cha hadithi ya “ **Walemavu barani Afrika**”, Kipindi kilichopita, Oluanda aliungana na walemavu wengine walioko Maganye na wote wakahiyari kufanya maandamano ya amani . Lakini katika kituo cha polisi, Gidi na Oluanda, viongozi wawili wa maandamano hayo, hawakufaulu kupata kibali kutoka kwa Inspekta Joe. Hivyo basi, lipi la ziada? Hebu tufuatilize, katika kipindi cha leo, “ **sio rahisi vile”.** Tunaanza hadithi yetu na Oluanda akiwaeleza kina Karemi na dadake Zabibu kuhusu mpango wake wa maandamano ya amani.

**<u>SCENE ONE : OUTSIDE KAREMI'S HOMESTEAD</u>**

**(ZABIBU IS SWEEPING THE COMPOUND WHILE SINGING)**

1. **SFX:** **BROOM SWEEPING LEAVES / DIRT**

2. **ZABIBU:** **SINGING**

3. **OLUANDA:** **(JOINS IN THE SONG)**

4. **ZABIBU:** Habari Oluanda, hata sikukusikia ukija.

**5. SFX:** **SOUND OF CRUTCHES APPROACHING**

6. **OLUANDA:** Nilitaka kuusikia wimbo wote hadi umalizike. Unaimba vizuri sana. Yuwapi Karemi? Amerudi kutoka shule?

7. **ZABIBU:** Ndio, yuko ndani. Ingia. Nyanya ameenda sokoni.

8. **OLUANDA:** Nataka nizungumze na nyinyi wawili. Alafu mutamueleza nyanya yenu atakaporudi.

9. **ZABIBU:** Hmm….Wajidai unkuwa mtu mzima, **(now smiling cheakily)** wataka kuoa, nini? Unajua tushasikia fununu kuhusu wewe na Kangwa.

10. **OLUANDA:** **(Chuckles)** Ah, watu wa Maganye wanayafuatilia sana maisha yangu. Lakini hapana, sio mwaliko wa harusi. Harusi bado.

Taafdhali mwambie Karemi aje? Ni vyema tuzungumzie hapa nje. Jioni ya leo yapendeza sana.

11. **ZABIBU:** Sawa. **(Calls out )** Karemiiiiii !... Oluanda anakuita!!!!

**12. MSIMULIZI:** Oluanda aliwaacha Karemi na Zabibu wakiwa na tama ya kujiunga na maandamano. Siku iliyofuata, uvumi kuhusu urafiki wa Oluanda na Kangwa, uilikuwa midomoni mwa watu. Wengi walishangaa. Vipi embe la dodo ligugunwe na popo? Au iweje mrembo kama Yule ampende mshona viatu tena kilema ? Oluanda alionekana amewavunja moyo wavulana wengi akiwemo Chitoto ambae alishindwa kujizuia shuleni.

**<u>SCENE TWO : BREAK-TIME AT SCHOOL</u>**

13. **SFX :** **SCHOOL BELL RINGS FOLLOWED BY NOISY STUDENTS**

14. **CHITOTO:** **(Calls out)** Kangwa! Kangwa!... **(Approaching)** Hebu tuongee hata kama ni dakika moja tafadhali. Umebeba nini mkononi?

15. **KANGWA:** Utaona. Unataka nini kutoka kwangu?

16. **CHITOTO:** **(Maliciously)** Hmm, Naona viatu vyako vinang'aa sana siku hizi. Labda nikusaidie kukupigia rangi wakati mwengine? Mimi si mshona viatu lakini…

17. **KANGWA:** Chitoto! Huwezi kuwa kama Oluanda.huwezi kumfika hata chembe.

18. **CHITOTO:** **(Loudly)** Kwa hiyo ni ukweli? Umechagua mwanamume mwenye kilema na kumuacha mwanamume kamili kama mimi?

19. **KANGWA:** **(Sarcastic)** Mwanamume kamili? Usinichekeshe . Chitoto, wewe bado ni mtoto unakua sasa. Haujakuwa wa kuitwa mwanamume.

20. **CHITOTO:** Unataka nini? Hmm… niambie nitakufanyie chochote ndio uamini….

21. **KANGWA:** Nataka uachane na mimi! Haya,ulisema unataka tuongee kwa dakika moja, tik tik ishaisha.

22. **MSIMULIZI:** Kangwa aliondoka, akamuacha Chitoto akijiuma midomo yake kwa hasira. Je, atakoma? Kangwa alielekea afisini kwa Bi.Nina kuomba ruhusa ya kuweka tangazo la maandamano ya amani katika ubao wa matangazo wa shule. Tusikilize yatakuwaje.

23. **SFX:** **GENTLE KNOCK ON DOOR**

24. **KANGWA:** Habari Bi. Nina, naomba kuingia ndani?

25. **BI.NINA:** Ndio, ingia Kangwa. Unatakaje?

**26.** **KANGWA:** Sio mengi. Ruhusa niweze kubandika arafa yangu .

27. **BI.NINA:** Sawa. Bandika tu kwa sasa nina kazi nyingi.

28. **KANGWA:** **(Excited)** Asante mwalimu..

29. **SFX :** **HURRIED FOOTSTEPS WALK DOWN A CORRIDOR**

30. **KANGWA:** **(Calls out)** Karemi!... Karemi, tafadhali njoo unisaidie.

31. **KAREMI:** Ni nini?

32. **KANGWA:** Nisaidie kubandika hii arafa kwenye mabandiko ya shule. Gundi ndio hii..

33. **SFX:** **CELOTAPE IS OPENED THEN CUT BY SCISSOR.**

34. **KANGWA:** Vyema, tuitoe hii nzee tubandike hiyo mpya, alafu uibandike hapo katikati ili kila mtu aione…

35. **SFX:** **PAPER BEING RIPPED APART FROM BOARD.**

36. **KAREMI:** **(Read out)** Waalimu wapendwa na wanafunzi, nyote munaalikwa kujiunga katika maandamano ya amani ili kuonyesha uzalendo na ndugu zetu walemavu hapa Maganye.

Maandamano yatakuwa Jumamosi. Msafara ukianzia sokoni, utapitia mjini kisha urudi tena ulipoanzia. Kuhudhuria kwako ni fanaka kwetu. Mwaliko huu umeletwa kwako na Oluanda. Mwanafunzi awali hapa, sasa mlemavu, na mwanaharakati.

37. **KAREMI:** Lo! Oluanda kweli ni mjasiri! Bila shaka utakuweko huko Kangwa.

38. **KANGWA:** Nitakuwa na Oluanda bega kwa bega. Babangu pia atakuja na hata mamangu pia..

39. **KAREMI:** Hivyo ni vizuri! Zabibu angelitaka kuja katika maandamano lakini vile itakuwa mchana hataweza kwa sababu ya jua . Lakini nyanyangu Theresa amesema atakuja. Ameahidi pia kumualika Porojo, yule muuguzi wa kienyeji na wazee wengine wa Maganye.

40. **KANGWA:** Vizuri sana! Basi tutapata uwakilishi wa kila sehemu. Siku hiyo itafana.

41. **SFX:** **SCHOOL BELL RINGS**

42. **MSIMULIZI:** Naam, kulingana na Kangwa mambo yalikua shuwari, wakati kengele ya kurudi darasani ilipopigwa, Oluanda na Gidi walikuwa hawako mbali kupata butwaa watakapokutana na Inspekta Joe kuhusu kibali cha maandamano yao. Inspekta anawasubiri na jawabu lao.

**SCENE THREE: AT MAGANYE POLICE STATION**

**43. SFX: POLICE STATION**

44. **GIDI:** **(Very upset )** Unamaanisha nini kuwa hutatupatia kibali?

45. **INSP.JOE:** Hivyo ndivyo wakubwa walivyoamuwa. Sina msaada mwengine wa kuwapatia.

46. **OLUANDA:** Wakubwa wako ni kina nani? Kwanini wametunyima kibali? Wanahofia nini? Hatuna nia ya kuiba wala kuvunja au kuharibu mali ya mtu yeyote!

47. **INSP.JOE:** Sikiliza, nimewaeleza yale nimeambiwa. Mimi nafuata maagizo.

48. **GIDI:** **(Cuts him short)** Maagizo! Hivyo ndivyo kawaida yenu munavyojibu. Njoo Oluanda, lazima tufikirie suluhisho la haraka na la kudumu. Labda kuna mtu wa cheo pahala Fulani hataki kilio chetu kisikike. Lakini kamwe hatuta rudi nyuma!

49. **INSP.JOE:** **( Threatening voice)** Kwa usalama wenu, mungeachana na hayo maandamano.. mukifanya hivyo itakuwa kinyume cha sheria na itabidi muchukuliwe hatua na sitakii kufikiria ni

nini itatokea.

50. **OLUANDA:** Sawa, Gidi. Uliyohofia yamekuwa. Tutakatiza maandamano. Tayari tuna matatizo yakutosha, haina haja kuongeza majeruhi na ulemavu zaidi kutokana na marungu ya askari walinda usalama.

51. **INSP.JOE:** Wazo zuri. Wazo zuri kabisa.

52. **MSIMULIZI:** Walihenga wahenga kuwa heri kuvunjika kidole kuliko kuvunjika moyo. Haya yalikuwa dhahiri katika nyuso za kina Oluanda na Gidi walipoondoka kituo cha polisi cha Maganye. Hawakuwa hata na nyuso za kuwatazamia wenzao. Wakashika njia kila mtu upande wake. Oluanda akarudi kazini kwake kushona viatu, Gidi akarudi sokoni. Baada ya hapo, siku hiyo mchana shuleni, Kangwa, ambaye alishazoea kupitia maskani ya Oluanda kila baada ya masomo, alimpitia Oluanda. Lakini safari hii aliandamana na babake Bw. Mali.

**<u>SCENE FOUR: OUTSIDE OLUANDA'S HOME</u>**

53. **SFX:** **OLD CAR ENGINE REEVES AND STOPS (FROM INSIDE CAR)**

54. **BW.MALI:** Ni yule aliyeketi pale kipembeni?

55. **KANGWA:** Ndiyo, ni yeye Oluanda. Anaonekana hana raha. Wacha nikutambulishe kwake.

56. **SFX:** **CAR DOORS OPENED AND CLOSED, FOOTSTEPS APPROACHING – OUTSIDE AMBIENCE**

57. **KANGWA:** **( Cheerfully)** Oluanda, habari gani? Niko na mtu ningelipenda umjue.

58. **BW.MALI:** Kwa kweli, kinyume na hayo.Ni mimi ndiye nilitaka kukujua.

59. **KANGWA:** Oluanda, huyu ni babangu, baba huyu ni Oluanda.

60. **OLUANDA:** Ni vizuri kukujua… karibu ukae..

61. **BW.MALI:** Unamaanisha usemayo? Kwa sababu sura yako inasema tofauti...

62. **KANGWA:** **(Shouts)** Baba!? **(lowers voice)** Oluanda Pole sana. Babangu anapenda sana matani. Lakini kama nilivyokwambia.. Anaunga mkono mpango wetu.  Na leo shuleni…

63. **OLUANDA:** Maandamano tuliyopanga yamesitishwa Kangwa.

64. **KANGWA:** **(Surprised)** Yamesitishwa? Kwanini ? Kila kitu kiko tayari.

65. **BW.MALI:** Kumetokea nini? Mbona munayahairisha dakika za mwisho?

66. **OLUANDA:** Sio mapenzi yetu, askari wametunyima kibali cha maandamano hayo, na hata wakatutishia.

67. **BW.MALI:** Nini? Huo ni mzaha. Muna kila haki ya kuwa na maandamano ya amani, munapigania haki zenu,ambazo mumenyimwa kwa muda mrefu.

68. **OLUANDA:** Kweli, lakini hatuna la kufanya. Wengi wa walemavu ni maskini na hatuna pesa kwa hivyo hakuna anayetaka kuzungumza nasi, licha ya kutusikiza.

69. **KANGWA:** Hii si sawa, hii si haki.

70. **BW.MALI:** La, maandamano hayatasitishwa wala kuahirishwa . Nitayafuatilia, nitazungumza na jamii ya wafanyi-biashara  na wanahabari, tutawaalika wanahabari kutoka ng'ambo kuinukuu siku hiyo. Alafu tuone kama watavunja maandamano hayo. Usife moyo Oluanda, mulipanda mbegu, sasa ni wakati wa kuimwagilia maji… hakuna ajuae mti huo utamea na kuwa mkubwa kiasi gani .

**HITIMISHO:**

Mambo yanazidi kuwa moto. Bw. Mali amemuhakikishia Oluanda kuwa yalipofikia sasa, ni mambo yao,  maandamano ya walemavu yamekua jambo la eneo zima na litavutia ulimwengu wa kimataifa. Je,hilo limetosha? Kumbuka Bi.Nina hajaisoma notisi iliyobandikwa shuleni kwake. Kweli atairuhusu shule yake kujumuika? Iwapo yataruhusiwa?

Na je, Bi. Mali atahisi vipi? Khususan atakapomuona binti yake anazidi kukaribiana na Oluanda?
Kwa majibu ya maswali haya na zaidi usikose kipindi chetu cha tisa kinachofuata. Kwa kusikiliza kipindi hiki au chengine, tembelea tovuti zetu www.dw-world.de/lbe. pia unaweza kutuma maoni au mawazo yako kuhusu haya yanayojiri. Kwa sasa tunakupa mono wa buriani.